

CLASS 5 END TERM 1 AUGUST 2021 KISWAHILI

ZOEZI LA 1: KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA

Mwalimu amwamkue mwanafunzi na kumwombwa ake. Mwalimu ajitambulisse.

"Mimi ni mwalimu _____ Niambie jina lako."
"Leo ningependa tuzungumze kuhusu nidhamu mezani."

1. Kuna ubaya gani mtu akila huku ameuacha mdomo ukiwa wazi?
2. Ni kwa nini tunapaswa kunawa mikono kabla ya kuanza kula?
3. Ukiwa na wenzako mezani na unahitaji chumvi upande wa pili, utafanya nini?
4. Eleza madhara ya kuzungumza unapokula.
5. Je, unadhani kula chakula kingi kupita kiasi mara moja kuna ubaya gani?

Alama
5

ZOEZI LA 2: KUSOMA KWA SAUTI.

Asubuhi hiyo, wanyama wote waliongozana kuelekea kisimani ili wakanawe nyuso zao na kuemsha kinywa kwa maji baridi mithili ya barafu. Kufika kisimani, lo! Hawakuamini macho yao. Kila mmoja alibaki amepigwa na butwaa kwani maji waliyotarajia kuwa safi yalikuwa machafu kupindukia. "Ni nani aliyetuchafulia maji yetu?" Mfalme simba aliliza kwa hasira nyingi. Walipotazama kwenye matope, waliona nyayo za mnyama mdogo. "Hebu nipisheni nizitazame nyayo hizo kwa makini," akasema nyani. Alipozitazama kwa karibu, alitambua mara moja kuwa mnyama aliyechafua maji alikuwa mnyama mdogo mwenye ujanja mwingi, masikio marefu na macho makubwa.

ZOEZI LA 3: KUSOMA KWA UFAHAMU.

Soma hadithi hii kisha ujibu maswali.

Alama
10

Tendo la kuheshimiana ni muhimu kwa wote. Wadogo wanafaa kuwaheshimu wadogo wao, marika yao na wakubwa wao. Wakubwa nao lazima wawaheshimu wadogo wao, marika yao na wakubwa wao. Tabia ya kukosa heshima huleta hali ya dharau kwetu sisi wanadamu. Je, Utafanya nini ili uweze kuheshimiwa? Ni lazima kama ibada uwaheshimu wengine ili nawe uheshimiwe. Ukitaka kudharauliwa na kila mtu, nawe mdharau kila mtu na ukumbuke kwamba ni tabia mbaya kuwadharau wenzetu. Heshima huanzia nyumbani ambapo mwalimu wa kwanza huwa ni mama. Baada ya kupokea mafunzo ya mwalimu huyo wa kwanza, sisi hutarajiwa kuendeleza heshima tukiwa shulenii.

1. Sentensi ya kwanza inaseme ni nini kilicho muhimu?
2. Tumeambiwa kuwa wakubwa wanafaa kuwaheshimu kina nani?
3. Kulingana na taarifa, kukosa heshima huleta hali gani?
4. Mwandishi anasema kuwa ukitaka kuheshimiwa ufanya nini?
5. Taarifa inasema kuwa mafunzo kuhusu heshima huanzia wapi?

ZOEZI LA 4: SARUFI

Chagua neno sahihi kujazia pingo.

barabarani saa safari miguu Mawingu

Maimuna alipoiangalia _____ yake mkononi, aligundua kuwa alibakiwa na
6

6

dakika ishirini tu kabla ya muda wake wa kufika nyumbani. mazito

7

yalikuwa yametanda angani. Labda mvua kubwa ingenyesha. Hakukuwa na gari lolote

8 kwa hivyo ilimbidi achape _____ hadi nyumbani. Alipoanza
9 _____, matone ya mvua yalianza kuanguka kwa hasira za mkizi.
10 _____

1

9

Eleza aina za maneno yaliyopigiwa mistari

11. Nilikula ndizi nne lakini sikushiba.

12. Ungeiona nyumba ya Bwana Rambo ungeitamani.

13. Wanyama wote walioshiba wamelala chini ya mti.

14. Paka aliyeumia mguu anatembea polepole.

Andika upya katika umoja au wingi

15. Joto limekuwa jingi.

16. Sikio halipiti kichwa.

17. Mipira ingeanguka mitoni.

18. Mtoto wa nyoka ni nyoka.

Kanusha sentensi hizi

19. Nilimba wimbo wa taifa kwa sauti.
20. Wewe umeichora bendera ya Kenya.

21. Yusufu anamnyoq kondoo.

22. Kina Kansiime wanaogelea kidimbwini.

Ambatanisha neno na kinyume chake.

- | | |
|--|--------|
| 23. Mfalme | utumwa |
| 24. Chuki | rafiki |
| 25. Adui | upendo |
| 26. Uhuru | malkia |
| <i>Andika katika hali ya mabanoni.</i> | |
| 27. Mti umekatwa. (udogo) | |
| <hr/> | |
| 28. Mtu anatembea. (ukubwa) | |
| <hr/> | |
| 29. Mbwa anabweka. (udogo) | |
| <hr/> | |
| 30. Mji umesafishwa. (ukubwa) | |

Alama
30